

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**112**

**SANAA UBUNIFU NA MICHEZO**

**MUDA: SAA 2:30**

**ALHAMISI 02 NOVEMBA, 2023 MCHANA**

**MAELEKEZO KWA MTAHINIWA**

1. Mtihani huu una sehemu TATU (3) A, B na C.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Jibu swali moja (1) kutoka sehemu C.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Tumia kalamu nyeusi au ya buluu kwa kuandikia na michoro iwe kwa penseli.
6. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

<b>KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI</b>		
<b>SWALI</b>	<b>ALAMA</b>	<b>SAINI</b>
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
12.		
<b>JUMLA</b>		
<b>SAINI YA MHAKIKI</b>		



023112708

**Mtihani huu una kurasa 9 zenye maandishi**

**SEHEMU A: (Alama 35)**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. Chagua jawabu sahihi katika kipengele (i) – (x) kisha andika herufi yake kwenye jadweli lililopo hapo chini.
  - i. Michezo ya riadha hujumuisha
    - A. Kukimbia, kuruka na kuogelea
    - B. Kukimbia, kurusha na kuruka
    - C. Kukimbia, kupika na kurusha
    - D. Kurusha, kuogelea na kupika
  - ii. Uchongaji ni njia moja wapo itakayomsaidia mtu kuweza
    - A. kupoteza mda
    - B. kujipatia kipato
    - C. kusaidia watu kazi zao
    - D. kufanya matembezi
  - iii. Zana zinazohitajika katika upishi wa ugali ni
    - A. maji, moto, sufuria, unga na mwiko
    - B. maji moto, unga, sufuria, samli na kijiko
    - C. maji, mwiko, kopo, chumvi na unga
    - D. mwiko, unga, moto, kopo na kijiko
  - iv. Moja kati ya ifuatayo ni msingi wa ujasiriamali
    - A. mfanyabiashara
    - B. mjasiriamali
    - C. mtaji
    - D. usafiri
  - v. Uokozi katika maji unahitaji vifaa maalumu. Vifuatavyo ni miongoni mwa vifaa vya uokozi **isipokuwa**
    - A. boya la uokozi
    - B. chuma cha uokozi
    - C. koti la uokozi
    - D. rafti ya kuokoa maisha

- vi. Moja kati ya ngoma zifuatazo **si** ngoma ya asili
- A. kidumbaki
  - B. msewe
  - C. msondo
  - D. zenji fleva
- vii. Mashairi hubeba sifa maalum ambayo hutambulisha kazi ya ushairi. Ni sifa ipi inayotambulisha kazi hiyo?
- A. kutumia kipaza sauti
  - B. kutumia lugha ya mkato
  - C. kutumia ngoma
  - D. kutumia vinanda
- viii. Ni utanzu upi wa fasihi ambao huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo ya wahusika?
- A. Ngoma
  - B. Riadha
  - C. Shairi
  - D. Tamthilia
- ix. Igizo la ubakaji ni mfano wa igizo lenye kulenga kuonesha jamii juu ya
- A. wizi
  - B. rushwa
  - C. udhalilishaji
  - D. burudani
- x. Maana ya kujitambua ni hali ya
- A. kuwatambua wengine katika jamii
  - B. kuwafahamu wengine katika jamii
  - C. kujifahamu mwenyewe na jamii husika
  - D. kutambuana katika jamii

**JAWABU**

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

2. Oanisha maelezo kutoka **kifungu A** kwa kuchagua jawabu sahihi kutoka **kifungu B** kama yanavyotumika katika mada ya huduma ya kwanza katika michezo. Andika herufi tu kwenye jadwali hapo chini.

KIFUNGU A	KIFUNGU B
i. Dalili na ishara za kuvunjika	A. Hakikisha usalama wako kwanza
ii. Hatua muhimu ya utoaji huduma ya kwanza	B. Huimarisha kinga ya mwili
iii. Kupoteza maji na chumvi chumvi mwilini	C. Ukosefu wa vitamin A
iv. Kula chakula bora chenye afya	D. Kukakamaa kwa misuli
v. Sababu za uvunjifu wa viungo vya mwili wa mwanadamu	E. Maumivu makali na uvimbe
	F. Dawa kumzowea mtumiaji
	G. Udhaifu wa mifupa

**JAWABU**

i.	ii.	iii.	iv.	v.

3. Andika **kweli** kwa maelezo yaliyosahihi au **sikweli** kwa maelezo yasiyosahihi katika jadwali liliopo hapo chini.
- Kufanya mazoezi bila ya kupumzika hupelekea kushuka kwa kiwango cha utendaji wa mazoezi kwa mwanamichezo.
  - Pipipili boga, keroti na hiliki ni viambaupishi vinavyotumika kupika muhogo.
  - Vigogo hutumika kutengenezea kinu na mchi.
  - Masoko **si** nyenzo muhimu sana kwa mjasiri amali.
  - Kuogelea kimgongomgongo humtaka muogeleaji kupiga miguu kama chura.
  - Njia nzuri ya kudhibiti fedha ni kuweka katika Taasisi za Kibenki.
  - Kuburudisha wahusika na hadhira ni moja ya umuhimu wa maigizo.
  - Mashairi ni kipande cha maandishi kilichopangwa kwa utaratibu maalumu.
  - Matayarisho ya jukwaa katika igizo hayahitaji ubunifu wa mandhari.
  - Vyakula vya protini huliwa na wanamichezo kwa wingi katika kipindi cha mashindano.

**JAWABU**

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

4. Jaza nafasi zilizowazi kwa kuchagua jibu sahihi.
- i. Mjasiriamali ni mtu anaeweza kuona \_\_\_\_\_ mbali mbali.
  - ii. Unga wa maandazi ni lazima ukandwe hadi \_\_\_\_\_ ili kufanya maandazi yawe laini.
  - iii. Kifaa hupakwa \_\_\_\_\_ baada ya kumaliza kuchongwa ili kivutie.
  - iv. Kwenye sekta ya bahari \_\_\_\_\_ ni kipaumbele cha kwanza.
  - v. Msaada wa haraka anaopewa alieumia au kupata jeraha kabla ya kufikishwa hospitali unaitwa \_\_\_\_\_

Vanish, fursa, uumuke, huduma ya kwanza, ulainike, hospitali, usalama.

**SEHEMU B: (ALAMA 45)**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

5. a. Elezea maana ya tamthilia.

---

---

---

- b. Taja aina tatu (3) za tamthilia.

---

---

---

- c. Andika njia tatu (3) za uandaaji wa tamthilia.

---

---

---

6. a. Elezea maana ya kuchonga.

---

---

---

- b. Taja vifaa sita (6) vinavyohitajika wakati wa kuchonga pamoja na matumzi yake.

Na.	KIFAA	MATUMIZI
i.		
ii.		
iii.		
iv.		
v.		
vi.		

7. a. Taja njia nne (4) za kiasili zinazotumika kuhifadhi chakula ili kisiharibike.

---



---



---



---

- b. Taja vifaa vitano (5) vinavyotumika kuhifadhia chakula.

---



---



---



---



---

8. a. Bwana Mkude ametoka Morogoro na kuja visiwani Zanzibar kujifunza kuogelea kwa ushindani. Eleza jinsi utakavyomfundisha kanuni tatu (3) za kuogelea kwa ushindani.

---



---



---



---



---



---



---



---

- b. Kwa ufupi elezea mitindo mitatu (3) ya kuogelea.

---

---

---

---

---

---

---

9. a. Nini maana ya mlo kamili?

---

---

---

- b. Taja aina tatu (3) za vyakula.

---

---

---

- c. Orodhesha madhumuni mawili (2) ya matumizi ya dawa.

---

---

**SEHEMU C: (Alama 20)**

**Jibu swali MOJA (1) katika sehemu hii.**

10. Vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vimekuwa vikiongezeka kwa kasi katika jamii yetu. Elezea njia nne (4) zitakazo punguza vitendo hivyo.
11. Timu ya taifa ya Zanzibar ilizuiwa kucheza fainali katika mashindano ya Afrika Mashariki kwa dhana ya kutumia madawa yasiyokubalika, baada ya uchunguzi ilithibiti sio kweli. Ili kuifunza jamii, fafania madhara matano (5) yanayoweza kupatikana kwa kutumia dawa zisizokubalika.
12. Yusra alikosa taaluma ya kutengeneza juisi ya Parachichi. Eleza hatua tano (5) anazoweza kuzifuata ili kutengeneza juisi hiyo.





**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.





